

**Heri ya Kuzaliwa**



**HAPPY BIRTHDAY**



**swahiliKIDS**

Jina langu ni Maria.

Leo ni siku yangu ya kuzaliwa.

Sasa najiandaa kwenda kitandani.

Kabla ya kulala, ngoja nikwambie kuhusu siku yangu.



My name is Maria.

Today is my birthday.

I am getting ready to go to bed now.

Before sleeping, let me tell you about my day



Leo ni siku ya furaha kubwa!

Asubuhi mama aliniletea kifungua kinywa kitandani.

-Chapati, mayai, maziwa, kipande cha embe na nanasi.



It's a joyful day today!

In the morning mom brought me breakfast in bed.

-Chapati, eggs, milk, a piece of mango and pineapple.

Mchana baba alitupekeka ufukweni  
kwenda kuogelea. Mimi na kaka yangu  
Tito tulichezea mchanga na maji mpaka  
tukachoka! Baadae tulipumzika kwenye  
kivuli chini ya mwavuli.



In the afternoon dad took us to the beach for  
a swim. My brother Tito and I played with the  
sand and water until we had enough! After  
that we rested in the shade under the umbrella.



Wakati wa kurudi nyumbani wazazi wangu waliniacha mimi na kaka yangu kwa shangazi Eva. Sisi tulifurahi sana kucheza na binamu zetu Imani na Baraka.



When going back home my parents dropped my brother and I at aunty Eva's place. We were so happy to play with our cousins Imani and Baraka.



Jioni baba alikuja kutuchukua. Aliponishika  
mkono nilianza kulalamika  
-Baba, kwanini unatuchukua mapema? Sitaki  
kurudi nyumbani. Bado nataka kucheza na  
binamu zangu. Natamani hata kulala hapa  
leo!



In the evening dad came to pick us up. When  
he held my hand I started whining-Dad, why  
are you picking us up this early? I don't want  
to go home. I still want to play with my  
cousins. I wish I could actually sleep here!



Baba alijibu kwa sauti ya chini-Hapana Maria! Huwezi kulala kwa shangazi leo mwanangu.

Kama vile hasikii kilio changu, baba aliaga harakaharaka,-Kwaherini wote. Muwe na jioni njema. Tutaonana wiki ijayo!.



Dad responded quietly, -No Maria! You cannot sleep over at your aunt's tonight. As if he didn't hear my cry, dad bid farewell quickly- Goodbye everyone. Have a great evening. We'll see you next week.

Ndani ya gari nilinuna njia nzima. Nilikataa kuongea kabisa. Tito alijaribu kunitania ili nicheke lakini nilikaa kimya. Siku yangu ilianza vizuri lakini leo ni siku mbaya kuliko zote maishani mwangu!



In the car I was mad the whole way. I refused to speak a word. Tito tried to say some jocks to make me laugh but I stayed silent. My day started well but today is the worst day of my life!



Tulipofika nyumbani, Tito alitangulia mbele.  
Alipofungua mlango nilishangaa kusikia kelele.  
Mara kundi kubwa la watu wakanikimbilia  
huku wakiimba-Heri ya kuzaliwa! Heri ya  
Kuzaliwa Maria!



When we got home Tito walked in front of  
me. As he opened the door I was surprised to  
hear some loud noise. All of the sudden a big  
group of people ran towards me singing-Happy  
Birthday! Happy Birthday Maria!

Baba alinibeba mabegani mwake.  
Nilipomtazama baba machoni, moyo wangu  
uliguswa. Nilimnong'oneza baba sikioni-  
Samahani sana baba. Sikufanya vizuri  
ulivyokuja kunichukua. Baba alijibu,  
nimekusamehe mwanangu. Nilimkumbatia baba,  
akanibusu kwenye shavu, kisha tukaingia ndani  
pamoja.



Dad carried me on his shoulders. When I  
looked him in the eyes, my heart was touched. I  
whispered on his ear-I am terribly sorry dad. I  
misbehaved when you came to pick me up. Dad  
responded, I have forgiven you my daughter. I  
hugged dad, he kissed my cheek, then we went  
inside together.



Sikujua mama aliniandalia sherehe ya kuzaliwa kwa siri! Mezani kulikuwa na keki nzuri, matunda, vyakula na vinywaji mbalimbali. Tulikula, kunywa, na kusherekea pamoja.



I didn't know mom had prepared a surprise birthday party for me! On the table there was a nice cake, fruits, a variety of foods and drinks. We ate, drank and celebrated together.

Nyumba ilijaa mapambo mazuri ya kuvutia. Maputo ya rangi nyeupe, njano, nyekundu, kijani, zambarau na waridi. Juu ya ukuta mama aliweka bango kubwa lililoandikwa-**HERI YA KUZALIWA MARIA!!!** Nilitabasamu kwa furaha.



The house was full of beautiful decorations. White, yellow, red, green, purple and pink balloons. On the top of the wall mom had put a big poster written-**HAPPY BIRTHDAY MARIA!!!** I smiled with joy.



Ndugu, marafiki na majirani waliniletea zawadi nyingi. Nilipokea vitabu, kadi, midoli, pipi na miwani ya jua. Asanteni sana wote kwa ukarimu wenu! Nilisema huku uso wangu umejaa machozi ya furaha.



Relatives, friends and neighbors brought me lots of gifts. I received books, cards, dolls, candy and sunglasses. Thank you so much everyone for your generosity! I said while my face was covered with tears of joy.

Nimefurahia sana siku yangu yakuzaliwa!  
Sasa naenda kulala huku natabasamu! Nalala  
huku nimemkumbatia mdoli wangu mpya Nana.  
Lala fofofu!



I have really enjoyed my birthday! Now I am  
going to sleep with a big smile on my face. I am  
sleeping while cuddling with my new doll Nana.  
Sleep tight!



Hivi ndivyo nlilivyosherehekea siku yangu ya kuzaliwa. Na wewe je? Siku yako ya kuzaliwa ni lini? Wewe unapenda kusherekeaje siku yako ya kuzaliwa?



This is how I celebrated my birthday. What about you? When is your birthday? How do you like to celebrate your birthday?

# UKUTA WA MANENO - WORD WALL

SWAHILI	ENGLISH
Busu	Kiss
Shavu	Cheek
Kumbatia	Hug
Nong'oneza	Whisper
Samahani	Sorry
Puto	Baloon
Zawadi	Gift
Keki	Cake
Bega	Shoulder
Pipi	Candy

# ZOEZI

Chagua jibu sahihi - Pick the correct answer

1. Maria anatimiza miaka mingapi?

- a. Kumi
- b. Ishirini
- c. Saba

2. Siku ya kuzaliwa tunasemaje?

- a. Heri ya pasaka
- b. Heri ya kuzaliwa
- c. Heri ya mwaka mpya

3. Kaka yake Maria anaitwa nani?

- a. Baraka
- b. Tito
- c. Imani

4. Imani na Baraka ni ...wa Maria

- a. Mjomba
- b. Shangazi
- c. Binamu

5. Maria alikula wapi kifungua kinywa?

- a. Sebuleni
- b. Kitandani
- c. Nje



# Watoto Mini Book Series by...



# swahili**KIDS**



**[SwahiliKIDS.com](http://SwahiliKIDS.com)**



**[@kiswahiliKIDS](https://www.facebook.com/kiswahiliKIDS)**



**[@swahiliKIDS](https://www.youtube.com/@swahiliKIDS)**



**[@swahili.KIDS](https://www.instagram.com/@swahili.KIDS)**